JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA MJI – NJOMBE

SHULE YA SEKONDARI MGOLA
S.L.P 786
NJOMBE
Mob 0759220830/0743000320/0759498008
……..

Barua pepe: mgolasec/@gmail.com
Kumb Na.MGOSS/JI/VOL 1/21.

Jina la mwanafunzi……

S.L.P……..

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MGOLA

1:0 Utangulizi
Ninayofuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka wa masomo 2021. **Shule ya sekondari Mgola** ipo katika H/MJI NJOMBE, Mkoa wa NJOMBE na umbali toka mji mkuu (Njombe Mjini) ni **30Km kusini mwa mji mkuu**.

Usafiri wa Basi kutoka mjini Njombe unapatikana katika kituo cha Mabasi **stendi mpya- Mji mwema** ikiwa nauli ni Tsh 5000/= muhula wa masomo unaanza tarehe 08/01/2021 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe hiyo na mwisho wa kuripoti ni tarehe 16/01/2021 ndani ya siku saba.

Mambo muhimu ya kuzingatia
2:1 (a) Sare za shule

WAVULANA
Mashati 2 meupe ya tetroni mikono mifupi na singlendi nyeupe 3, suruali 2 damu yam zee (angalia kitambaa), viatu vya ngozi vyeusi kisigino kifupi jozi 2 vyenye kamba. Sweta za bluu 2 zenye mshono wa V shingoni, soksi jozi 2 za khaki nyeusi, suruali 2 nyeusi, T-shirt nyekundu 2 (isiyo na maandishi au picha) kwa ajili ya kazi, Tracksuti nyeusi, tai damu ya mzee, Pulneki nyeupe tatu (3) na Mopa 1 yenye mshikio mrefu (Mfagio wa kukaushia maji).

WASICHANA
Suruali 2 rangi damu ya mzee (angalia kitambaa) mshono wa suruali za kike, visolo/vigauni vidogo 2 damu ya mzee vinavyoishia kwenye magoti vyenye rinda box (rinda kubwa mbele na nyuma) mikono mifupi, mashati 2 meupe mikono mifupi. Sweta za blue 2 zenye mshono wa v shingoni, sketi nyeusi 2, sketi ya kijani, Pulneki nyeupe 3, viatu vyeusi kisigino kifupi jozi 2, soksi nyeupe jozi 3, tracksuit nyeusi 2, fulana 2

nyekundu au njano, bajaji jozi 1 kwaajili ya kuvaa wakati wa kazi, kanga au kitenge doti moja na Brush ngumu 1 yenye mshikio mrefu ya kusugulia sakafu.

NB: SARE ZOTE ZIWEKWE ALAMA YA KUDUMU

(b) Rangi ya hijab ni nyeupe (kwa waislam)

(c) Sare ya michezo kwa shule hii ni raba 2 na bukta 2 rangi ya njano au nyekundu kwa wavulana na bukta 2 rangi ya kijani inayobana kwenye mapaja na raba jozi 2 kwa wasichana.

2.2 Bunda moja la karatasi (RIM A4), Daftari kubwa 10 (3quire), daftari ndogo 9 zenye kurasa 48 kwa ajili ya mazoezi ya kila wiki, kalamu za wino, rula (inayo angaza), mkebe wa hesabu (mathematical set), faili na dictionary (kamusi ya kiingereza).

2.3 Gharama za uendeshaji wa Hosteli (Daharia) na matibabu

AINA YA MCHANGO	**MUHULA WA KWANZA**	**MUHULA WA PILI**	**JUMLA KWA MWAKA**
MAHINDI	DEBE 6	DEBE 6	DEBE 12
MAHARAGE	DEBE MOJA NA NUSU	DEBE MOJA NA NUSU	DEBE 3
MCHELE	KILO 10	KILO 10	KILO 20
FEDHA YA UENDESHAJI WA HOSTELI	TSH. 73,000/=	TSH. 73,000/=	TSH. 146,000/=
MATIBABU (HUDUMA YA KWANZA)	TSH.2,500	TSH. 2,500/=	TSH.5,000/=
JUMLA KUU YA FEDHA	75,500	75,500/=	151,000/=

NB: *Fedha zote zilipwe kwenye akaunti ya shule* **NO. 60610003637** NMB **MGOLA SEKONDARI**.

HATUTAPOKEA FEDHA TASLIMU HAPA SHULENI TULETEE HATI YA MALIPO (BANK PAYING IN SLIP).

2.4 Mpe mwanao nauli ya kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo

2.5 Mahitaji mengine ya kibinadamu,

(a) kwa kila nguo ya ndani ziwe zaidi ya 4 kwa wavulana na zaidi ya 6 kwa wasichana

(b) Godoro imara na madhubuti futi mbili na nusu **(Mfano QFL –DODOMA)**, blanketi 2, nzito, shuka 2 za pink na mto 1.

(c) Vyombo vya kulia chakula (sahani, bakuli, kikombe na kijiko),

(d) Aje na kufuli na sanduku imara (Tranka) kwa ajili ya kutunzia vitu vyake.

(e) Vifaa vya usafi binafsi (sabuni, kiwi, mswaki na dawa yake, brashi, ndoo 1 ya lita 10 na taulo).

(f) NB: Hakikisha unamfungulia mwanao BIMA YA AFYA iliyoboreshwa ili kurahisisha matibabu ya mwanao akipelekwa hospitali au Zahanati za serikali ndani ya mkoa wa Njombe
(Kadi ya bima Aje Nayo).

3:0 Sheria na kanuni muhimu za shule.

3.1 Shule inaendeshwa kwa mjibu wa sheria ya elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyoboreshwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha vile vile inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzi ya ufundi yenye dhamana na Elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la

usimamizi na uendeshaji Elimu kwa hiyo mwanafunzi (mwanao) anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote na wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Kushiriki kikamilifu katika maandalio ya jioni (Night preparation)
c) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani au nje ya mipaka hiyo wakati wote wauanafunzi.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule kwa ujumla.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote uwapo hapa shuleni na kutunza mali za umma

3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya vilevile uvutaji bangi coceine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu mali ya umma kwa maksudi
g) Kudharau bendera ya taifa
h) Kuoa au kuolewa
i) Kupata mimba au kusababisha mimba au kushiriki na/kutoa mimba
j) Kugoma au kuchochea au kuongoza mgomo au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule/watu.
k) Kukataa adhabu kwa maksudi
l) Kuwa na simu ya mkononi shuleni

4:0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni

a) (Medicala Examination Form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maendeleo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

5:0 Kikao cha wazazi/walezi kitafanyika tarehe 06/02/2021 siku ya jumamosi kitakachoanza saa 4:00 asubuhi. Hudhuria bila ya kukosa.

6:0 Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA MGOLA SEKONDARI

MKUU WA SHULE

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PRESIDENTS OFFICE- RALG

NJOMBE TOWN COUNCIL

MGOLA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 786,
NJOMBE.
DATE……..

THE MEDICAL OFFICER,

……

Please examine ……..

As to Her/His fitness for pursuing further education at this school.

1. Hemoglobin ……
2. P.V. Bleeding ……
3. (a) Sight ……
   (b) Hearing ……
4. Blood pressure ……
5. Urine for sugar and pregnancy tests …… ……
6. Stool for routine examination ……
7. Asthma ……
8. Skin diseases ……
9. Leprosy ……
10. Epilepsy ……
11. Pulmonary tuberculosis ……
12. Deformity ……
13. Mental problem ……
14. Comments ……

……

MEDICAL OFFICER

TAARIFA ZA MWANAFUNZI NA KIAPO

A . TAARIFA ZA MWANAFUNZI.

1. **JINA ULILOTUMIA TOKA SHULE ZA MSINGI……**
2. **DINI YAKO/DHEHEBU……**
3. **JINA KAMILI LA BABA/ MLEZI ……**
   KAZI YAKE ……
   ANWANI YAKE ……
   NAMBA ZA SIMU …… AU……
   MAHALI ANAPOISHI: MKOA …… WILAYA……
   TARAFA …… KATA……KIJIJI/MTAA……

4. **JINA KAMILI LA MAMA / MLEZI ……**
   KAZI YAKE ……
   ANWANI YAKE……
   NAMBA ZA SIMU …… AU ……
   MAHALI ANAPOISHI : MKOA …… WILAYA……
   TARAFA …… KATA……KIJIJI/MTAA……

5. **TAJA NDUGU WENGINE WA KARIBU SANA**

S/N	JINA KAMILI	UHUSIANO	ANAPOISHI	NAMBA YA SIMU
1				
2				
3				

(B) KIAPO

6. KWAMBA MimiMwanafunzi…… naapa/nakirikuwataarifahizi nizakwelinanitatiisheria , kanuninataratibuzashulekamanilivyofahamishwa mudawoteniwapomwanafunzi.

SAHIHI YA MWANAFUNZI …… TAREHE ……

6. **KWAMBA Mimi …… (Mzazi/Mlezi) naapa/ nakirikuwanakubali sharia, kanuninamaelekezoyoteyaliyotolewanayatakayotolewanauongoziwashule.**

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI ……TAREHE……

TAARIFA HII IRUDISHWEKWA MKUU WA SHULE.